# ARUSHA

## FURSA LUKUKI

#Endless Opportunities

Toleo la Mtandaoni: 01 Tarehe 28/11/2022



#Kazi Iendelee

**UTALII, KILIMO, BIASHARA NA UZALISHAJI**





**Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan akiwatunuku Kamisheni Maafisa Wanafunzi 724 wa JWTZ katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli - Arusha.**
**tarehe 26/11/2022**




**Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan akifungua Mkutano wa 27 wa Jumuiya ya Wanasheria Afrika Mashariki Mkoani Arusha.**






**Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Jumuiya ya Wanasheria Afrika Mashariki mara baada ya kufungua Mkutano wa 27 wa Jumuiya hiyo Mkoani Arusha.**



# BILIONI 520 MRADI WA MAJI ARUSHA NA VIUNGA VYAKE

Rais Samia Suluhu Hassan ahaidi kutatua changamoto za Maji,Soko na Barabara kwa Wilaya ya Arumeru baada ya Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi Noah Lembris kuelezea adha wanazozipata Wananchi wa Jimbo lake.

Akizungumza wakati wa hitimisho la Ziara ya Rais Mkoa Arusha,Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi Lembris alimweleza Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Wananchi wa Mji mdogo  wa Kisongo wanachangamoto ya Soko la Kisasa kwani kwa miaka mingi eneo hilo linatumika kama Mnada ambao unakusanya Watu wengi hivyo kuwepo kwa umuhimu wa kujengwa Soko la Kisasa litakalosaidia Halmashauri kukusanya Mapato kwa wingi vilevile kukidhi mahitaji ya Wanan chi wa Maeneo ya Mji mdogo wa Kisongo.

Sambamba na hilo,Mhe. Lembris alimwomba Mhe. Rais asaidie kutatua changamoto ya Barabara za ndani toka kwenye maeneo ya uzalisha pamoja na kutatua kero ya Maji kwani Tanki lililopo kwa sasa ha liwezi kukidhi mahitaji ya Wananchi wa Maeneo ya Mji mdogo wa Kisongo.

Akitoa maelekezo ya Serikali Mhe.Rais ameiagiza Ofisi ya Rais -TAMISEMI kuhakiksha Soko la Kisasa linajengwa lenye kukidhi mahitaji ya Wananchi,sambamba na kuwapa TARURA jukumu la kupitia maombi hayo ya Barabara za ndani ili kutatua changamoto hizo.

Kwa upande wa Maji Mhe. Rais amehaidi kupitia Mradi Mkubwa wa AUWSA una ogharimu Bilioni 520 kuwafikishia huduma ya Maji Wananchi hao wa eneo la Mji mdogo wa Kisongo.

Kwa Upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-TAMISEMI Profesa Riziki Shemdoe amesema wao kama TAMISEMI wamepokea maelekezo ya Mhe. Rais na kuhaidi kuyashughulikia kwa kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Arusha kuandaa andiko la Mradi wa Soko ili waweze kuingiza katika mpango wa bajeti 2022/2023.

Aidha kwa Upande wa kero ya Barabara Katibu Mkuu Shemdoe amesema watakwenda kukaa na TARURA ili kuona Arumeru inaongezewa pesa katika bajeti ya TARURA kwaajili ya kutatua changamoto ya Barabara hizo.

**Rais Samia Suluhu Hassan amemaliza ziara yake ya siku nne Mkoani Arusha kwa kusimama eneo la Kisongo na kuzungumza na Wananchi kwa kusikiliza kero mbalimbali zinawakabiri.**



**Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Wanachi wa Mji mdogo wa Kisongo Wilayani Arumeeru mara baada ya kumaliza ziara yake ya kikazi ya siku 4 Mkoani Arusha akiwa njiani kuelekea Dodoma**



**Viongozi wa Chama na Serikali wakimuaga Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan mara baada ya kumaliza Ziara yake ya kikazi Mkoani Arusha.**

# MRADI WA MAJI, KIKWE



## MTUE MAMA NDOO

Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella amewataka wananchi wa kijiji cha Kikwe kuutunza na kuulinza mradi wa Mji waliojengewe na serikali kupitia Wakala wa Maji na usafi wa Mazingira Vijijini(RUWASA).

Ameyasema hayo alipokuwa akikagua mradi huo wa Maji uliojengwa kwa gharama ya zaidi ya Milioni 202 na watu takribani 5,430 watanufaika na mradi huo.

Mongella amesema serikali imewekeza fedha nyingi katika mradi huo ili kusogeza karibu huduma ya maji kwa wananchi na kuwapunguzia hadhi ya kutafuta maji umbali mrefu.
Hivyo wananchi hao wanatakiwa kuutunza na kuulinda ili uweze kuwanufaisha kwa muda mrefu.
Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Richard Ruyango, amesema wao kama viongozi wa Wilaya watahakikisha mradi huo unalindwa na kutwanza kwani Serikali ya Mama Samia imewekeza fedha nyingi kwa lengo la kutatua changamoto ya wananchi ya kufuata Maji umbali mrefu.

Kwa upande wake mwenyekiti wa kamati ya watumia maji Kijiji cha Kikwe bwana Orwa Alexander amesema mradi huo utawasaidia wananchi kifikishiwa maji hadi kwenye makazi yao kwa kulipia gharama ndogo.
Amesema lengo lao ni kuhakikisha kila mwanakijiji anapata maji nyumbani, hivy wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi wengine ambao bado hawajauwelewa mradi vizuri.

Amemshukuru Rais Samia Suluhu kwa kuwaletea maji atika kijiji hicho kwani mradi ulitangulia ulikufa kutokana na usimamizi mbovu ila kwa sasa Serikali imewaletea mradi mpya ambao wanausimamia wenye wananchi kwa uwangalizi wa RUWASA.

Nae, Diwani wa Kata ya Kikwe Daniel Kaaya amemshukuru Rias Samia kwa kuleta fedha hizo zilipelekea wakapata mradi huo wa maji ambao wananchi wananufaika nao kwani kabla ya mradi walikuwa wanatumia Maji machafu ya mito ila kwasasa wanapata Maji safi na Salama.



**"Dhamira ya Serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan nikutatua chaangamoto zinazo wakabili wananchi wake, ikiwemo uhaba wa Maji. Huu ni ushahidi tosha kuwa kazi inaendelea"**

JOHN V.K MONGELLA



# MIRADI YA BARABARA



## Mianzini–Sambasha–Ngaramtoni

Zoezi la kupisha ujenzi wa barabara ya Mianzini hadi Ngaramtoni kwa kubomoa nyumba zote zilizopo ndani ya mita 10 kila upande mwisho wake ni Disemba 26,2022.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella alipokuwa akikagua ujenzi wa barabara hiyo katika halmashauri ya Jiji la Arusha na Arusha.

“ Serikali imeshaleta fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii, haiwezekani ikacheleweshwa na watu wachache wasiotaka kubomoa nyumba zao”,alisema. Aidha, ameitaka Wakala wa barabara Tanzania (TANROAD) kuendelea kutoa elimu ya sheria ya barabara kwa wananchi ili waweze kuifahamu vizuri na kujenga uelewa wa pamoja.

Mongella amesema kwa mujibu wa sheria ya barabara ya mwaka 2007 upana wa barabara ulitakiwa kuwa mita 20 kila upande lakini serikali ya Rais Samia inayowajali wananchi wake na haitaki wapate kero hivyo imepunguza na kuwa mita 10 kwa kila upande.

Amewataka wananchi wa maeneo ambayo barabara hiyo inapita, kuunga Mkono juhudi hizo za serikali kwani barabara inaleta maendeleo. Pia, amewataka wananchi kuchangamkia fursa hiyo ya ajira wakati ujenzi huo ukiendelea.

Kwa upande wake, Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Arusha Muhandisi Regnand Massawe amesema barabara hiyo ya Mianzini Sambasha ina urefu wa KM 12 na ile inayoanzia Olemringaringa hadi Ngaramtoni ina urefu wa KM 6.

Amesema barabara hiyo kwa ujumla ina urefu wa KM 18 na itagharimu Bilioni 22 hadi kukamilika kwake na kwa sasa ujenzi umefikia 8%.
Matarajio ya kukamilika kwa mradi huo ni mwaka Agosti 2023 ikiwa umeanza Agosti 2022.









# UTIAJI SAINI MIKATABA YA BARABARA, TARURA

Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella amewataka wakandarasi waliosaini mikataba ya kutengeneza Barabara wakafanye kazi kwa weledi, uzalendo na kuzikamilisha kwa muda uliopangwa.

Ameyasema hayo alipokuwa akishuhudia utiaji saini wa mikataba kati ya Wakala wa barabara vijijini na Mijini ( TARURA) na wakandarasi takribani 18 kwa Mkoa wa Arusha.

Katika hatua hiyo ya kusaini mikataba Mongella amewataka wakandarasi hao wakafanye kazi zenye viwango.

Amesema,kwa kukamilisha barabara hizo kwa wakati na kwa viwango kutasaidia kushusha gharama za maisha kwa wananchi.za mikataba 34 ilisainiwa yenye thamani ya bilioni 14 sawa na 60%.

Aidha, amewaelekeza TARURA wakawasimamie wakandarasi hao kwa ukaribu zaidi ili wakamilishe miradi hiyo kwa wakati.

Pia, amewataka wakasimamie miradi ya barabara ya zamani ili nayo iweze kukamilika haraka.

Kwa upande wake, Katibu Tawala Mkoa wa Arusha Missaile Musa amesema, kwa kitendo cha wakandarasi kusaini mikataba hadharani kitasaidia wananchi kuwafahamu wakandarasi watakaoenda kufanya kazi katika maeneo yao.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Arusha Lynas Sanya amesema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 walipatiwa jumla ya fedha za matengenezo ya barabara zaidi ya bilioni 18 kwa awamu ya pili na katika awamu ya kwan

Awamu ya pili ya utiaji saini umewekwa katika mikataba 18 yenye thamani zaidi ya bilioni 4.07 sawa na 40%.

Amesema,kwa mwaka wa fedha 2022/2023 TARURA katika bajeti yake wamepatiwa zaidi ya bilioni 10 fedha zilizotokana na tozo za mafuta ili zikasaidie katika ukarabati wa barabara katika Mkoa wa Arusha.

Nae, Mkandarasi Rashidi Sevingi kutoka kampuni ya Raly (EA) Limited amewahasa wakandarasi wengine kwenda kutekeleza mikataba waliyosaini kwa weledi ili waendelee kuaminiwa zaidi na Serikali.

TARURA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 wamesaini Mikataba 52 yenye thamani ya bilioni 18 kwa ajili ya ukarabati wa barabara mbalimbali za Mkoa wa Arusha.





# KIKAO CHA BODI YA BARABARA

Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella amezitaka halmshauri zote Mkoani hapo kupitia Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na Wakala wa barabara Tanzania(TANROAD) kumaliza barabara zote zinazojengwa kwa umbali wa Kilomita 1 kukamilika ifikapo Januari, 2023.

Ameyasema hayo alipokuwa akifungua kikao cha 46 cha bodi ya barabara Mkoa wa Arusha.
"Hakuna haja ya kutumia muda mrefu kujenga barabara zenye kilomita 1 na kuwafanya wananchi kukosa huduma".

Miundombinu ya barabara ni kichocheo muhimu cha kujenga uchumi wa wananchi na nchi kwa ujumla.
Amesema, serikali imeongeza bajeti ya barabara kwa kiasi kikubwa ili kura hisishabarabara kukamilika kwa wakati, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 TARURA wamepatiwa fedha kiasi cha bilioni 18.2 na kwa mwaka 2021/2022 bajeti ilikuwa bilioni 9.
Kwa upande wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) bajeti ya mwaka 2021/2022 ilikuwa Milioni 13 na kwa mwaka wa fedha 2022/2023 bajeti ni milioni 12.9 kwa mtandao wa barabara wa kilomita 1,493.12 kwa kiwango cha lami na changalawe.

Amewataka viongozi wa Wilaya na Halmshauri kwenda kusimamia na kufahamu mitandao ya barabara iliyopo katika maeneo yao.
bodi ya barabara Mkoa kimefanyika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023.

# NYUMBA YA WAGENI



**Mkuu wa Mkoa Wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akiwa katika mazungumzo na Balozi wa Saudi Arabia Nchini Mhe Abdullah Aisheriyan alipofika kumtembelea ofisini kwake.**



**Mkuu wa Mkoa Wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akiwa katika mazungumzo na Balozi wa Sweden Nchini Tanzania Mhe. Charlotta Macias, ambaye aliwasili Mkoani Arusha kwa ziara ya kikazi.**



**Mkuu wa Mkoa Wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akiwa katika mazungumzo na Waziri wa Katiba na Sheri Mhe. Dkt Damas Ndumbaro alipowasili Mkoani Arusha kwa ziara ya kikazi.**



**Mkuu wa Mkoa Wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akitete jambo na Kamisaa wa Sensa Mhe. Anna Makinda.**